# MWONGOZO KWA WAALIMU WA WATOTO WADOGO KATIKA SHULE YA JUMAPILI



UTUMIWE NA WAALIMU WA WATOTO WADOGO UMRI WA MIAKA 4, 5, 6

# MWONGOZO KWA WAALIMU WA WATOTO WADOGO KATIKA SHULE YA JUMAPILI

Utumiwe na waalimu wa watoto wadogo

umri wa miaka 4, 5, 6

Mwongozo huu umetayarishwa hasa kutumiwa wakati wa mkazo wa

"Mwaka wa Shule ya Jumapili"

©

Copyright, 1985
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI, KENYA

## YALIYOMO


Utaratibu wa Shule ya Jumapili .................................. 2

Kusudi na Kazi za Shule ya Jumapili .............................. 3

Mgawo wa Watoto Wadogo .................................. 4

Mwalimu wa Shule ya Jumapili .................................. 7

Kulitayarisha Somo .................................. 9

Vifaa vya Kufundisha .................................. 11

Njia za Kufundisha .................................. 12


Utaratibu wa Jumapili Asubuhi .................................. 15

Kutembelea .................................. 16



# MWONGOZO KWA WAALIMU WA WATOTO WADOGO KATIKA SHULE YA JUMAPILI

"Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu" (Luka 2:52). Hatujui mengi kuhusu utoto wa Yesu. Lakini twajua kwamba Yusufu na Mariamu walimfundisha habari za Mungu. Tena, alifundishwa Maandiko hekaluni. Huu ndio mfano wetu. Ni lazima tuwafundishe watoto wadogo habari za Mungu kanisani na nyumbani.



Katika Biblia yote tunasoma juu ya mpango wa Mungu wa kufundisha. Soma Mithali 22:6, Kumbukumbu la Torati 4:9-10; 31:12-13. Haya ni maagizo ya Mungu kwetu. Viongozi wa kanisa hawana budi kutimiza wajibu wa kuwafundisha watoto wadogo.

Katika makanisa ya Kibatisti, darasa la Shule ya Jumapili ndiyo mahali pema zaidi pa kuwafundisha watoto wadogo. "Nilipokuwa mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga, nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga..." (Wakorintho 13:11). Mtoto mdogo hawezi kuelewa mambo ambayo watoto wakubwa wanaweza kuelewa, kwa hivyo ni lazima kuwa na darasa ambalo ni la watoto wadogo--wenye umri wa miaka 4, 5, na 6. Maelezo ya kitabu hiki yatawasaidia kufahamu jinsi ya kuwafundisha watoto wadogo.

# UTARATIBU WA SHULE YA JUMAPILI

Shule ya Jumapili ni sehemu ya kanisa.

1. *Viongozi wa Shule ya Jumapili* wanachaguliwa na kanisa. Kwa kawaida, Shule ya Jumapili ina viongozi wafuatao:

   a. Msimamizi — Yeye hupanga kazi ya Shule ya Jumapili. Husaidia kuwafunza waalimu.

   b. Mwandishi — Yeye huweka rekodi ya wale wanaohudhuria.

   c. Waalimu — Kila darasa litakuwa na mwalimu. Kazi yake itakuwa kufundisha darasa lake siku ya Jumapili, kuwatembelea nyumbani siku za wiki, na kuwasaidia washiriki kukua katika maisha ya kiroho. Kila darasa linapasa kuwa na mwalimu msaidizi pia.

2. *Migawo ya Umri*


   Inapasa kuwepo madarasa ya migawo ifuatayo:

| | |
|---|---|
| Watoto Wadogo | (umri wa miaka 4-6) |
| Vijana Wadogo | (umri wa miaka 7-12) |
| Vijana | (umri wa miaka 13-21 |
| Watu Wazima | |

Kama kanisa linavyozidi kukua, madarasa mengine yanaweza kuongezwa. Tafadhali, soma Ukurasa 3 wa kitabu cha *Kukuza Makanisa Yako kwa Njia ya Shule ya Jumapili.*

3. *Siku ya kuwapandisha wanafunzi juu* au kuwahamishia katika darasa lililo mbele katika Shule ya Jumapili ni jambo muhimu sana kwa watoto wote. Jambo hili si gumu, lakini linahitaji mpango. Kila kanisa linapaswa kutenga siku moja maalum ya kuwapandisha watoto juu. Siku nzuri ni Jumapili ya kwanza ya mwaka mpya. Pili, mweka mipaka ya umri kwa kila darasa. Kwa mfano, darasa la Watoto wadogo linapasa kuwa na watoto wenye umri 4-6 pekee. Siku ile ambayo kanisa limeweka, wale watoto walio na umri wa miaka saba watakwenda katika darasa la Vijana Wadogo (Primary Class). Wale Vijana Wadogo na Vijana nao watabadilisha madarasa yao wakati watakapofikia umri wa kutosha.

4. Kila darasa litahitaji *mahali pa kukutania.* Labda wanaweza kukutania kanisani, chini ya mti au katika nyumba iliyo karibu. Kanisa ni lazima kukata shauri juu ya mahali ambapo kila darasa litakutania.



5. Kanisa pia litaweka *wakati au saa ambayo Shule ya Jumapili inapasa kukutana.* Kwa kawaida, ni saa moja kabla ya ibada kuanza. Walakini, kila kanisa linaweza kujiwekea wakati linaloona kuwa unafaa. Ni muhimu kuanza mafunzo wakati uliowekwa na kumaliza wakati uliopangwa.

## KUSUDI NA KAZI ZA SHULE YA JUMAPILI

Kusudi la Shule ya Jumapili ni kuwafikia watu wote kwa ujumbe wa Kristo. Hili pia ni kusudi la mwalimu wa watoto wadogo. Ingawa watoto wadogo hawawezi kuelewa dhambi na wokovu, mwalimu wao ana nafasi nzuri sana kuwaambia wazazi na jamaa zao.

Kuna kazi muhimu tano za Shule ya Jumapili:

- *Kuwafikia watu wa jamii*
- *Kuwafundisha Biblia*
- *Kuwavuta kwa Kristo*
- *Kuwakuza kuwa Wakristo wenye imara*
- *Kuwasaidia mahitaji yao*

Je, mwalimu wa watoto wadogo awezaje kutimiza kazi hizo? Je, zinazo maana gani kwako?

1. *Kumfikia mtoto mdogo katika jamii* — Kwanza, jaribu kuwaandikisha watoto wadogo wote wenye umri kuanzia 4 hadi 6 walio watoto wa washiriki wa kanisa lako. Kisha, uwaalike watoto wale ambao wazazi wao si washiriki wa kanisa lako. Utahakikisha kwamba wanafika na kurejea nyumbani salama. *Mtoto chini ya umri wa miaka 4 asifike bila mzazi.*

2. *Kuwafundisha Biblia* — Watoto wadogo WANAWEZA kujifunza Biblia. Hili ni jambo muhimu sana. Biblia inatuamuru kumfundisha mtoto mdogo. Kumbuka kifungu kisemacho: "Nilipokuwa mtoto mchanga nalifahamu kama mtoto mchanga..." (1 Wakorintho 13:11). Watoto wadogo wanaweza kufahamu upendo wa Mungu na ulinzi wake kwao. Tambua ya kwamba WANAWEZA kujifunza. Wafundishe katika njia wanazoweza kuelewa.

3. *Kuwavuta kwa Kristo* — Ni kweli kwamba watoto wadogo hawaelewi na dhambi, toba na wokovu. Kwa hivyo, wajibu wako ni kujenga msingi wao wa kufahamu. Wafundishe ya kwamba Mungu anawapenda. Watakapokuwa wakubwa wataelewa ya kwamba kwa sababu Mungu anawapenda na atawasamehe wataweza kumpokea na atawaokoa.

4. *Kuwakuza kuwa Wakristo Wazima* — Hapa tena, mwalimu wa watoto wadogo atakuwa akijenga msingi. Wasaidie kuelewa na mambo haya: kanisa ni mahali pa kumwabudia Mungu; Biblia ni kitabu maalum; maombi ni kuzungumza na Mungu anayewafahamu na kuwapenda.

5. *Kuwasaidia mtoto mdogo na jamaa yake* — Tembelea nyumbani kwa mtoto mdogo ili uweze kufahamu mahitaji yake. Kweli, watoto wadogo huwa na shida. Unaweza kuonyesha upendo na huruma. Pia utakuwa na nafasi kuwafahamu jamaa za watoto. Unaweza kuwaalika kuhudhuria Shule ya Jumapili na ibada. Pia, unaweza kushiriki nao ushuhuda wako.

## MGAWO WA WATOTO WADOGO

Mgawo huu ni kwa watoto ambao hawajaanza shule ya msingi. Sasa uzidi kufikiria mpango kwa mgawo huu.

1. *Mgawo wa watoto wadogo* unaanzia watoto waliozaliwa hadi wakati wanapoanza shule ya msingi. Kwa kawaida kuingia shule, watoto watakuwa na miaka sita au saba, au hata zaidi. Walakini, katika makanisa mengi, madarasa ya watoto wadogo sana hayapo. Watoto wadogo sana hutunzwa tu na ndugu zao wakubwa, au wakati mwingine huingizwa katika

madarasa ya watoto wadogo wenye miaka 4 hadi 6. Makusudi haya yote mawili siyo mazuri. Wakati wa mafunzo ya Shule ya Jumapili, watoto ambao wana umri wa miaka 1, 2, na 3, wanapaswa kutunzwa na watu wazima. Ikiwa kanisa linaweza kuwa na darasa lingine kwa watoto wadogo sana, basi ni vema. Lakini ikiwa halina, watoto hao wakae na wazazi wao wenyewe. Katika Shule ya msingi ya serikali, mtoto asingeruhusiwa kuja na ndugu yake mdogo, kwa sababu asingeweza kusikiliza na kujifunza vyema. Kwa hivyo, wakati wa mafunzo ya Shule ya Jumapili, wazazi wanapaswa kuwatunza watoto wao wadogo sana ili watoto wao wengine waweze kujifunza.

2. *Darasa la watoto wadogo* ni la watoto wenye umri wa miaka 4,5, na 6. Watoto hawa ni wa nasari. Wanaanza tu kujifunza.

## Tabia za Mtoto Mdogo

Katika mwongozo huu, tutajifunza juu ya mtoto aliye na umri wa miaka 4-6. Tutajifunza jinsi anavyotenda na anavyojifunza.

1. Yeye ni mtendaji. Anakua; anahitaji kunyosha viungo vyake. Anapenda kujenga na kuchora. Anapenda kutembea na kupiga ngoma. Anapenda KUFANYA matendo.



2. Uwezo wake wa kuangalia ni mfupi. Husikiliza vyema kwa wakati mfupi tu. Ingawa anaweza kukaa kimya, pengine hasikilizi. Anaweza kufikiria jambo moja tu, kwa wakati mmoja. Ukimwonyesha picha wakati unaposimulia hadithi, labda ataacha kufikiria na ataanza kufikiria juu ya picha ile.

3. Hujifunza kwa kutumia hisi zake. Huhitaji kugusa vitu pamoja na kuona na kusikia. Ni vyema zaidi akiweza kunusa na kuonja vitu. Mpe vifaa vya mafunzo ambavyo anaweza kugusa kama maua na vifaa vingine kama picha kubwa.

4. Huzungumza kwa sentensi rahisi, kwa hivyo uzungumze naye katika lugha rahisi anayoweza kuelewa. Hawezi kuelewa mawazo kuhusu

mambo ambayo hawezi kuona au kusikia au kugusa. Kwa mfano ingekuwa vigumu kwake kuelewa maana ya imani. Anaweza kuelewa uzuri wa maua ambayo anaweza kuona kuliko uzuri wa ulimwengu mzima. Labda ingekuwa vizuri kuzungumza naye katika kilugha chake wanachotumia nyumbani. Ingawa Kitabu cha Mwalimu kinaweza kuchapishwa katika lugha tofauti, utahitaji kutumia lugha ambayo wanaelewa.

5. Ni mwenye kujifikiri binafsi. Hujipendeza yeye mwenyewe. Daima hutumia maneno "mimi," na "changu." Ni vigumu sana kwa mtoto kushirikiana na watoto wengine vitu vyake. Kushirikiana katika michezo kwa kusubiri zamu yake ni hatua ya kwanza ya kushirikiana na wengine vitu vyake.

6. Hupenda kuiga. Mtoto hutaka kuwa kama mwalimu. Onyesha jinsi ya kuwatendea wengine wema kwa kuwa mwema na mvumilivu.

**Sababu za Kumfundisha Mtoto Mdogo**

1. Mafunzo ya mapema ni muhimu. "Nusu ya mambo yote ambayo mtu hujifunza katika maisha yake, atakuwa amejifunza kabla ya kupita umri wa miaka mitano." Hilo ni kweli! Kila kanisa lahitaji kutoa mafunzo ya kiroho kwa kila mtoto.

2. Mungu hutuamuru kuwafundisha watoto wadogo. "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6). Kanisa halina budi kutimiza agizo hili. Hii ni ahadi kutoka kwa Mungu yenye agizo, yaani, "Kama mtoto akifunzwa, atakumbuka mafunzo hayo." Kanisa lina wajibu wa kuwafunza watoto wadogo.

3. Watoto wadogo wanayo mahitaji yao muhimu. Kanisa linaweza kusaidia kuongoza na kufundisha umuhimu wa mambo ya kiroho kuhusu mahitaji hayo.

a. Hitaji la kwanza maishani mwa mtoto mdogo ni *upendo*. Huhitaji kupokelewa. Kama mtoto akipendwa, ataonyesha imani kwa anayempenda.

b. Mtoto huhitaji *uongozi*. Watoto wote huhitaji kujifunza ya kujitawala. Hujifunza kushiriki, na kuwaheshimu wengine. Mwalimu huongoza na kusimamia matendo ya mtoto darasani.

c. Mtoto huhitaji kujifunza jinsi ya *kujitegemea*. Hujifunza kutengwa na jamaa yake wakubwa kwa wakati mfupi.

d. Mtoto huhitaji kukuza moyo wa *kujiheshimu* na kujiona kuwa mtu wa thamani. Yeye ni kiumbe maalum kilichoumbwa na Mungu.

e. Ili kuwa na ujuzi wa kujifunza na kukua, mtoto mdogo huhitaji kujaribu mambo mbalimbali ambayo atafaulu kwa mengine na kushindwa kwa mengine pia. Mwalimu atakuwako pale kumsaidia na kumtia kila mtoto moyo.

## Njia ambazo Mtoto Mdogo Hujifunza

1. Mtoto hujifunza kwa kupatwa na ujuzi halisi. Hujifunza kwa kutenda. Fanya mpango kwa matendo ambayo yatamsaidia mtoto kujifunza. Fundisha kwa kutumia mchezo wa kuigiza na matendo mengine.

2. Mtoto hujifunza kwa njia ya michezo. Mtoto anaweza kuwazia mambo mengi. Pengine atawazia ya kwamba mbao ni gari, na maua ni chakula. Kwa njia ya michezo mtoto hujifunza kushiriki na kufanya kazi na wengine.

3. Mtoto hujifunza kwa njia ya muziki. Hukuza uwezo wake wa kulinganisha sauti mbalimbali za nyimbo na kuziimba. Mfundishe kuonyesha furaha na shukrani zake kwa Mungu kwa njia ya nyimbo au muziki. Tumia vyombo vingine vya muziki. Tunga nyimbo pamoja na watoto.

4. Mtoto hujifunza kutokana na mifano ya watu wazima: wazazi wake, mchungaji, na mwalimu wake wa Shule ya Jumapili. "Mtoto hawezi kujifunza Biblia mwenyewe; anaweza tu kujifunza jinsi uso wako unavyoonekana, kuhisi maono yenu, na matendo yenu." Mtoto atajifunza kutokana na vitu anavyoona ukifanya wala siyo mambo tu. Atajifunza anayosikia ukisema.

# MWALIMU WA SHULE YA JUMAPILI

Je, unaamini kwamba Mungu amekuita kuwa mwalimu wa watoto wadogo kama vile alivyomwita mchungaji kuhubiri? Wewe ni sehemu muhimu sana ya kazi ya kanisa.

### Masharti ya Mwalimu wa Watoto Wadogo

Waalimu wengine hufikiri kwamba kufundisha Darasa la Watoto Wadogo si muhimu kama kufundisha watoto wakubwa. Hili si wazo la kweli. Mwalimu wa watoto wadogo ana kazi muhimu SANA kufanya. Kwa hivyo, mwalimu mwema ni lazima atimize masharti hayo:



1. Mwalimu mwema atakuwa mwaminifu kujifunza Biblia na kuomba kila siku. Hawezi kufundisha mambo asiyoyajua. Pia, awe mwaminifu katika kuhudhuria kanisa.

2. Ni lazima awapende watoto na kutaka kuwafundisha. Watoto hutambua mara moja ikiwa mwalimu anawapenda.

3. Kumbuka: Mwalimu hufundisha kwa mfano. Mwalimu mwema atakuwa mwaminifu na mwenye haki.

4. Mwalimu asitarajie kulipwa mshahara. Kufundisha katika Shule ya Jumapili ni njia ya kumtumikia Mungu. Mwalimu ni lazima kuwa wakili mwema na wakati wake na uwezo wake.

**Kazi za Mwalimu wa Watoto Wadogo**

1. Jitayarishe mwenyewe kwa njia ya maombi na mafunzo ya Biblia. Mwalimu hana budi kukubali kujifunza na kutayarisha somo kila wiki. Ajaribu kuhudhuria mafunzo yote (semina) ya Shule ya Jumapili.

2. Tembelea nyumbani kwa wanafunzi. Kufanya hivyo kutakusaidia kuwafahamu jamaa za wanafunzi pia. Utapata nafasi nzuri ya kumfahamu mtoto pamoja na mahitaji yake.

3. Fika mapema siku ya Jumapili. Mwalimu ni lazima kuwa darasani kumwamkia mtoto wa kwanza kufika.

4. Kuwa mwaminifu kuhudhuria. Kumbuka kwamba unafundisha kwa mfano. Ikiwa huhudhurii mara kwa mara, watoto hawatajifunza kwamba Shule ya Jumapili ni muhimu.

5. Jifunze somo na ufanye matayarisho yahitajiwayo. Unahitaji kuandika mpango wa somo na kutayarisha vifaa utakavyotumia.

6. Jua majina ya watoto. Jambo hili litamfanya mtoto kujiona kwamba anapendwa na kupokelewa.

7. Weka rekodi ya wale wanaokuja. Tumia daftari kuandika majina ya watoto. Kila wiki, uwatembelee watoto ambao hawakufika mafunzoni.

8. Fundisha kutoka kwa Biblia. Unapaswa kutumia kitabu cha Mwalimu nyumbani kujiandaa. Ni vyema kuandika mpango wa somo kila wiki. Lakini wakati wa darasa, tumia Biblia. Kumbuka kwamba mtoto hujifunza kwa kuona na kusikia. Anahitaji KUONA ukifundisha kutoka kwa Biblia.

## KULITAYARISHA SOMO

1. **Maombi ... kwa ajili yako mwenyewe,** kwa ajili ya watoto wa darasa lako na kwa ajili ya wazazi wao.

2. **Anza mapema** katika wiki (Jumatatu) kulitayarisha somo. Soma somo lote lililo katika kitabu cha Mwalimu.

3. **Soma maandiko ya Biblia.** Soma tena maelezo ya Biblia katika kitabu cha Mwalimu.

4. Andika kusudi la somo. Jibu swali hili, "Je, ninataka watoto kujifunza nini kutoka kwa somo hili?"

5. Andika mpango wa kufundisha somo. Mpango huo umedokezwa katika kitabu cha Mwalimu. Unaweza kuufuata au unaweza kufanya mabadiliko mengine. Andika mpango wako; hii itakusaidia kukumbuka mpango ule siku ya Jumapili.

6. Panga matendo ya watoto kufanya. Kumbuka kwamba watoto hujifunza kwa njia ya kutenda. Kutakuwa na matendo yatakayodokezwa kila wiki katika kitabu cha Mwalimu. Mambo mengine yameelezwa katika kitabu hiki. Fanya matendo hayo kuwa sehemu ya mpango wako.

7. Jifunze kifungu cha kukumbuka na nyimbo za kuimba. Mfano wako wa kujifunza kifungu hicho cha kukumbuka utawatia watoto moyo. Nyimbo zinadokezwa kwa kila somo. Uzitumie; zimeandikwa hasa kwa ajili ya watoto wadogo.

8. Jifunze kusimulia hadithi ya Biblia. Hiki ndicho kiini cha somo kwa watoto wadogo. Tumia madokezo katika kitabu hiki. Ujifunze kusimulia hadithi vizuri. USIWASOMEE watoto hadithi tu, bali uwasimulie kama kwamba ni hadithi yako mwenyewe.

9. Tayarisha vifaa vyo vyote vya mafunzo na ukusanye vifaa vingine utakavyotumia: picha, vitu, mawe, karatasi za kuchorea, n.k.

Andika mpango wa kila wiki katika daftari. Jibu maswali haya:

Je, naweza kuanza kwa jinsi gani?
Je, tutaimba nyimbo gani?
Je, nitasimulia hadithi lini?
Je nitatumia michezo gani?
Je, somo hili lina maana gani kwa watoto wadogo wa darasa langu?



## VIFAA VYA KUFUNDISHIA

Vitabu vya masomo vya Shule ya Jumapili ya Kibatisti vimetayarishiwa kwa waalimu wa watoto wadogo.

"Kuwafundisha Watoto Wadogo" ni kitabu cha Mwalimu ambacho kimeandikwa kutumiwa katika makanisa madogo. Ni kitabu kifupi kinachohitaji vifaa vichache vya kufundishia.

Kila kitabu kina masomo 13 ambayo yanatosha kwa miezi mitatu. Masomo hayo yamegawanywa katika mifululizo mitatu ya masomo. Kila mfululizo wa masomo wahusu jambo moja.

Picha za watoto kupeleka nyumbani zina hadithi upande wa pili. Hadithi hii ni sawa na ile inayopatikana katika kitabu cha Mwalimu. Picha hizi za watoto zimekusudiwa kutumiwa na kitabu cha Mwalimu.

Picha kubwa zenye rangi pia zinapatikana. Picha hizi ni sawa na zile za watoto kupeleka nyumbani, lakini hizi zitumiwe na mwalimu kama kifaa cha mafundisho yake.

Upate habari kutoka Baptist Publishing House kuhusu vitabu na vifaa vingine vinavyopatikana katika nchi yako. Katika Tanzania agiza kutoka Baptist Literature Centre, SLP 1240, Moshi, Tanzania.

## NJIA ZA KUFUNDISHA

Mojawapo ya kazi ya Shule ya Jumapili ni kufundisha Biblia. Je, ina maana gani kwa watoto "kujifunza Biblia?" Kwa mtoto kujifunza kweli za Biblia pekee haitoshi. Ni lazima ajifunze kwamba Biblia ina maana kwa maisha yake. Soma Kumbukumbu la Torati 6:6-9. Wazazi (na waalimu) wanaambiwa kuwafundisha watoto kweli za Biblia mchana wote wakati watoto wanaposaidia katika kazi ya nyumbani. Mtoto anaweza kuona kwamba Biblia ina maana kwa maisha yake. Katika darasa la Shule ya Jumapili, mwalimu anapaswa kupanga matendo ili mtoto anaweza kujifunza wakati anapotenda. Baadhi ya matendo yanayoweza kutumiwa ndiyo hayo yafuatayo:

1. *Kusimulia hadithi* — Wakati unapojitayarisha katikati ya wiki, soma hadithi ya somo mara kadhaa. Jifunze kutamka majina ya watu na mahali yanayotajwa katika hadithi hiyo. Wakati unaposimulia hadithi, tumia maneno rahisi. Tumia maneno yenye kuonyesha matendo na uyarudie ili kukaza hadithi. Kwa mfano, kwa mkazo ungeweza kusema, "Basi mtu yule akatembea, akatembea, akatembea." Uketi wakati wa kusimulia hadithi ili uwe sawa sawa na watoto. Uwatazame watoto macho kwa macho. Ufungue Biblia kwa maandiko unayotumia unapofundisha. Lakini, usiwasomee hadithi. Mara kwa mara ubadilishe sauti yako. Tumia mikono yako, uso, na hata miguu. Wakati unaposimulia utumie mazungumzo mengi iwezekanavyo kati ya watu fulani katika hadithi.






2. *Picha* — Picha huwasaidia watoto KUONA hadithi vizuri. Walakini, usiwaonyeshe picha wakati unaposimulia hadithi. Waonyeshe picha kabla ama baada ya kusimulia hadithi. Weka picha sawa sawa na watoto waweze kuiona kwa urahisi. Waulize maswali juu ya picha hiyo.

Njia nyingine za kutumia picha:


a. Soma kifungu cha Biblia. Waambie watoto wachague picha moja kati ya picha zile, ambayo wanafikiri inafaa.


b. Weka picha kadha chumbani. Mnong'onezee mtoto juu ya picha moja. Mwambie akate shauri ni picha gani uliyomwelezea, kisha mwulize aende akasimama karibu na picha ile. Rudia mtindo huu mpaka picha zote zimechaguliwa.






3. *Muziki* — Watoto wote hupenda kuimba. Ni vizuri kutumia muziki wakati wa kuwafundisha watoto. Walakini, msiimbe *tu.* Nyimbo ziimbwazo zinapaswa kuwa na maana kwa mtoto. Muziki ni njia ya kufundisha. Jaribu kutumia nyimbo zilizo katika kitabu cha Mwalimu. Nyimbo hizi zimeandikwa kwa ajili ya watoto wadogo. Maneno ya nyimbo hizi ni rahisi tena yanaeleweka vizuri. Unaweza kutumia sauti yo yote. Labda utahitaji kutafsiri maneno hayo katika lugha ambayo watoto wanaelewa. Watoto wanaweza kuonyesha furaha na shukrani kwa Mungu kwa njia ya muziki. Kuimba pia ni njia moja ya kuwaongoza watoto wafanye matendo na pia kutembea chumbani. Waambie wapige makofi na kujongeza miguu yao. Wanaweza kutengeneza ala za kutumia.





4. *Mchezo wa kuigiza* — Watoto wanapenda sana kuigiza hadithi. Hawahitaji kufanya mazoezi au kuwa na nguo maalum. Waongoze kukumbuka hadithi na kuigiza. Watoto wengine wajifanye kuwa jua, wengine mwezi, wengine nyota, wengine maua na miti, na wengine watu.

5. *Matembezi Nje* — Imetajwa ya kwamba watoto hujifunza kwa kuona, kugusa, na kutenda. Wanaweza kuelewa zaidi habari za muumbo wa Mungu wakiona viumbe vyake Mungu. Matembezi hayo yafanywe katika eneo la kanisa na yatumie dakika tano au kumi hivi. Wafundishe watoto kuona uzuri wa ulimwengu. Watajifunza kufikiri habari za Mungu na viumbe vyake. Wafundishe kuutunza ulimwengu wao. Kwa mfano, Wasichume maua yote ya mti, wasikanyage mimea mipya; wasivunje matawi ya miti michanga, n.k.




6. *Mazungumzo* - Ni sehemu muhimu sana ya kuwafundisha watoto. Watoto hujifunza kwa kutenda; wao husikiliza mafunzo kwa wakati mfupi tu. Hupenda sana kuzungumza. Wape nafasi kueleza mawazo yao. Wasikilize. Ujifunze jinsi wanavyosikika mafunzo.

7. *Kuchora* kunawapa watoto njia ya kuonyesha mawazo yao. Wape vifaa vya kuchorea, yaani, karatasi, kalamu za rangi, au magazeti na makaa; chaki ya kuandikia ubaoni, matawi ya ndizi na vijiti, au mahali pa kuchorea mchangani na vijiti. Haya yote yanaweza kutumiwa kuwapa njia za kuchora.

8. *Maombi* — Mtoto anahitaji kufahamu kwamba maombi ni muhimu. Watoto watajifunza kwamba kuomba ni kuongea na Mungu wakati wanapoona mfano wako. Labda mwalimu aseme, "Ninajisikia kuwa na moyo wa kumshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki zangu. Je, mngependa kuomba?" Watie watoto moyo kuomba. Watumie mawazo yao wenyewe na maneno. Usisahihishe maombi ya mtoto.

Maombi mengi ya watoto ni ya shukrani. Mwalimu anapaswa kutumia maneno rahisi wakati anapoomba. Aombe maombi mafupi tu ya sentensi tatu au nne tu.

**Waambie watoto wajitoe kuomba kwa hiari.** Usimlazimishe mtoto kuomba ikiwa hataki. Kila mtoto anayetaka kuomba apatiwe nafasi kufanya hivyo.



## UTARATIBU WA JUMAPILI ASUBUHI

1. Ufike mapema. Tayarisha mahali pa kukutania na umkaribishe kila mtoto anapowasili. Tandika mikeka au matawi ya ndizi ili waketi. Unaweza kutumia mikeka au matawi kama mkikutana ndani au nje. Mwalimu pia aketi juu ya mkeka au matawi au kiti kidogo, lakini asiketi juu kuliko watoto.

2. Ufuatao ni mfano wa mpango wa somo unaoweza kufuata:

MFULULIZO WA MASOMO: Marafiki Kanisani
SOMO HILI: Paulo na Lidia
KUSUDI: Kuwasaidia watoto kuelewa kwamba wana marafiki kanisani.
KULIFUNDISHA SOMO:
Makaribisho: Sema, "Mariamu ni rafiki yangu. Nafurahi ya kwamba umefika hapa leo."
Wimbo: "Napenda kwenda Kanisani"
Rekodi: Wakati unapoita jina la kila mtoto, mtoto yule asimame. Weka alama katika daftari yako kando ya majina ya watoto ambao wamefika. Watoto wote wakiwa wamesimama, waimbe.
Wimbo: "Napenda kwenda Kanisani." Mtembee darasani wakati mnapoimba.

Kifungu Cha Biblia: Weka vipande vya karatasi ndani ya Biblia yako katika vifungu vilivyodokezwa. Mwambie mtoto mmoja achague karatasi. Sema "Nimeweka alama katika Biblia kuonyesha kifungu kinachotuambia habari za marafiki. Nitasoma kifungu hicho ambacho rafiki yangu, 'Mariamu', amechagua." Soma vifungu vitatu au vinne, watoto wakichagua makaratasi.

Wimbo: "Marafiki"

Mazungumzo: Zungumzeni juu ya urafiki.

Hadithi ya Biblia: Fungua Biblia yako katika Matendo 16. SIMULIA hadithi ya Paulo na Lidia.

Matendo: Fanyeni mchezo wa kuigiza hadithi hiyo. Labda unaweza kwenda nje na watoto na kujifanya kwamba mnakutana kando ya mto kama Paulo alivyofanya. Waonyeshe watoto picha hiyo.

Wimbo: "Marafiki"

Kifungu cha Kukumbuka: Sema, "Ninyi ni marafiki zangu" Yohana 15:14. Waambie watoto wakariri kifungu hicho.

Maombi: Mshukuru Mungu kwa marafiki.

Wimbo: "Rafiki Yangu Mkubwa ni Yesu"

## KUTEMBELEA

**Mojawapo ya kazi za Shule ya Jumapili ni kuwafikia watu. Tembelea nyumbani mwa watoto wa darasa lako. Kufanya hivyo kutadhihirisha upendo wako kwa watoto wako na kwa wazazi wao. Watie jamaa zao moyo kuhudhuria Shule ya Jumapili. Ikiwa wazazi wao si Wakristo, labda unaweza kuwashuhudia.**



Mwalimu anapaswa kutembelea nyumba za:

1. kila mtoto, mara mbili au zaidi kila mwaka.
2. kila mtoto anayekosa kufika darasani siku ya Jumapili.
3. kila mtoto baada ya kuhudhuria kwa mara ya kwanza.
4. kila mtoto ambaye wazazi wake hawahudhurii.
5. kila mtoto anayekaa karibu na hahudhurii Shule ya Jumapili yo yote.

## MWISHO

**"Yesu akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabariki" Mark 10:16. Yesu alifundisha kwa kutumia vitendo vilivyofuatwa na maneno. Aliwapenda watoto akawabariki. Watoto hujifunza juu ya upendo wa Mungu na Biblia ikiwa mwalimu anawapenda na kuwafundisha.**